Familia na Watoa huduma Wapendwa,

Kusoma huanza wakati mtoto anapozaliwa! Ni muhimu kwamba familia zihisi kuwa zinaungwa mkono na zijue jinsi zinaweza kuwahimiza watoto kusoma utotoni mwao. Tumeandaa kifurushi hiki ili kukupa baadhi ya maelezo na mwongozo kuhusu jinsi unaweza kuwasaidia watoto kusoma na kujiandaa kufanikiwa katika shule ya chekechea.

Jamii yetu imefanya kazi kwa pamoja ili kukupa baadhi ya rasilimali muhimu, ikiwa ni pamoja na orodha ya ujuzi, ambayo itakupa dhana kuhusu jinsi ya kuwasaidia watoto kujiandaa kufanikiwa katika shule ya chekechea. Rasilimali ya thamani zaidi kwa watoto ni familia au watoa huduma wao, na muda uliotumika kwa pamoja na wahusika hawa katika kusoma, kugundua mambo na kufurahia utoto wao! ***Ijapokuwa ujuzi uliorodheshwa ni mapendekezo, si lazima watoto waweze kufanya kila kitu kwenye orodha ili kuanza masomo ya shule ya chekechea.***

Mafunzo haya yana maelezo mbalimbali yanayohusiana na kuwaandaa watoto kufanikiwa katika shule ya chekechea, yale watoto watakuwa wakisoma katika shule ya chekechea na mambo ya kufurahisha ambayo mnaweza kufanya pamoja ili kukuza na kuunga mkono ujuzi wa watoto! Miongozo sita kutoka kwa Idara ya Elimu ya Michigan ambayo inaangazia baadhi ya maswali ambayo wazazi wanaweza kuwa nayo wakati watoto wao wanaingia shule ya chekechea yamejumuishwa katika mafunzo haya. Miongozo ya ziada inaweza kupatikana kwenye http://www.michigan.gov/mde/0,4615,7-140- 6530_6809-152726--,00.html.

Tungependa kuhakikisha kwamba watoto wote (na familia na watoa huduma) wamejiandaa kufanikiwa katika shule ya chekechea. Kwa kufanya kazi kwa pamoja tunaweza kufanya haya kuwa ya kufana na ya kufurahisha kwa kila mtu!

Wako mwaminifu,

Kamati ya Ushauri wa kuwa Tayari Kuanza Shule (The School Readiness Advisory Committte)
Kikundi cha Ingham Great Start Collaborative

Nyenzo hizi zilitengenezwa na ruzuku iliyotolewa na Idara ya Elimu ya Michigan na Idara ya Elimu ya Marekani.

Watoto hujifunza ujuzi mwingi tofauti katika maeneo yafuatayo ambayo utawasaidia kujiandaa kufanikiwa katika masomo ya shule ya chekechea. Baadhi ya ujuzi huu ni pamoja na:

Ukuzaji wa Lugha

- **Kujibu maswali kuhusu hadithi mlizosoma pamoja**
- **Kuweza kushiriki mara moja au zaidi katika mazungumzo**
- **Kutumia maneno aliyojifunza kutoka kwa hadithi, maisha yake na mazungumzo**
- **Kuweza kueleweka na watu wengi wakati anaongea**
- **Kutumia maneno kama mimi, yeye na yake kwa njia sahihi.**

Ukuzaji wa uwezo wa Kusoma na Kuandika

- **Kutamka sauti katika maneno (kutia vina, sauti za kuanza)**
- **Kutambua herufi kubwa 18 na herufi ndogo 15 na baadhi ya sauti herufi zinazotoa**
- **Kugundua jina lake mwenyewe lililoandikwa**
- **Kuangalia kitabu kuanzia mbele hadi nyuma na kupindua kurasa moja baada ya nyingine**
- **Kuandika jina lake la kwanza linaloanzia kwa herufi kubwa na kumalizia na herufi ndogo.**

Ukuzaji wa Hesabu:

- **Kuhesabu hadi 20 kwa sauti**
- **Kuashiria kwa kidole na kutumia jina moja la nambari kwa kila kitu anachoashiria kuanzia 1 hadi 10**
- **Kutambua nambari 1-10**
- **Kutambua maumbo msingi (mraba, mviringo, pembetatu, almasi, umbo yai n.k.).**
- **Kuunda mpangilio wa sehemu mbili (kijani, nyeupe, kijani, nyeupe).**
- **Kupanga vitu kulingana na sifa ambayo vitu hivyo vinashirikiana kwa pamoja (rangi, ukubwa, umbo n.k.)**

Kukua Kimwili

- **Kuruka kwa miguu miwili**
- **Kutumia mshiko wa tripodi (kidole gumba na vidole viwili) kuandika au kuchora herufi, nambari au umbo**
- **Kutumia makasi ya watoto**

Ukuaji wa Kijamii

- **Kuwaamini watu wazima na watoto wengine**
- **Kucheza na, si kando tu, bali kucheza pamoja na watoto wengine**
- **Kujifunza na kushiriki katika kikundi**

Kukua Kihisia

- **Kuwa mbali na mtoa huduma msingi kwa kipindi kirefu**
- **Kushughulikia mahitaji yake ya kibinafsi (k.m. kujipanguza baada ya kwenda choo, kunawa mikono)**
- **Kudhibiti maonyesho ya hisia zao**
- **Kufahamu nafasi binafsi yao wenyewe na ya wengine**

Njia ya Kusoma

- **Kuonyesha tamaa na msukumo wa kusoma mambo mapya**
- **Kutumia dakika 10-15 kufanya kazi kwa kijitegemea**
- **Kulenga na kuzingatia shughuli kwa dakika 10-15 (k.m. kusikiliza hadithi)**
- **Kukumbuka na kuunganisha uzoefu na mazingira (duka la mboga, maktaba)**
- **Kufuata maelekezo ya hatua mbili na kukumbuka taratibu rahisi**
- **Kufuatilia na kutatua matatizo rahisi (k.m. kutatua fumbo)**

Nyenzo hizi zilitengenezwa na ruzuku iliyotolewa na Idara ya Elimu ya Michigan na Idara ya Elimu ya Marekani.

Ninaweza Kufanya Nini Nyumbani?
Mwongozo wa Wazazi #16

Kama mwalimu wa kwanza wa mtoto wako una jukumu kubwa. Unaweza kumsaidia mtoto wako kujiandaa kwenda shule na kufanikiwa maishani.

Wingi na ubora wa muda uliochukua kushughulikia masuala ya mtoto wako ni muhimu sana. Unaweza kufanya mambo kadhaa ili kumsaidia mtoto wako kujiandaa vyema kwenda shuleni huku bado akifurahia.

- **SOMA Naye kila siku.** Shiriki upendo wako wa vitabu na mtoto wako. Utafiti unaonyesha kuna faida za kumsomea mtoto wako kwa dakika 30 kila siku. Si lazima kuifanywe mara moja.
- **ONGEA na SIKILIZA.** Unapoongea na kumsikiliza mtoto wako, anajifunza lugha na ujuzi anaohitajika.
- **MANENO Tumia maneno mengi kadri uwezavyo ili kufafanua vitu katika ulimwengu wa mtoto wako.** Idadi ya maneno ambayo mtoto wako anayajua yanahusiana na ufanisi wake wa baadaye wa kusoma. Usitumie 'matamshi ya kitoto'. Mtoto wako akikosea kisarufi, rudia neno kwa usahihi.
- **HESHIMA.** Kuwa na heshima kwa mtoto wako na wengine. Mtoto wako hujifunza kwa kukuangalia. Hakikisha matendo yako ni yale ambayo ungetaka mtoto wako arudie.
- **CHEZA na watoto wako.** Waruhusu watoto wakuone kama mtu anayeweza kucheza nao. Kumbuka kwamba kucheza *ni* kazi ya mtoto. Watoto hutatua matatizo na kujifunza ujuzi mpya kupitia kucheza.
- **MSAIDIE mtoto wako kujiona kama mtu mwenye uwezo.** Msaidie mtoto kuweza kujiamini kwa kuonyesha mtoto wako vitu vyote anavyovifanya kuwa ni 'vizuri.' Fanya juhudi ya kutafuta mambo mazuri katika mtoto wako.
  Msaidie mtoto wako kuona jinsi yeye ni mzuri
- **PIKA na mtoto wako.** Pima, mwaga, koroga, soma mapishi, safisha, na ule pamoja na mtoto wako. Shughuli za kupika ni njia nzuri ya kufanyisha misuli midogo mazoezi.. Misuli hii hutumika baadaye kuandika.
- **PAKA RANGI na chora na mtoto wako.** Hii itaboresha ujuzi wake wa kutembea na kusaidia kuandaa misuli kwenye vidole ili kuandika.

OMBA usaidizi. Ikiwa una wasiwasi kuhusu kukua kwa mtoto wako katika eneo lolote, na mtoto yuko chini ya umri wa miaka mitatu, piga simu kwa 1-800-*Early On*. Ikiwa mtoto wako ana umri wa zaidi ya miaka mitatu, wasiliana na Build Up Michigan (http://buildupmi.org), wilaya ya shule ya eneo lako, au Idara ya Elimu ya Michigan, Ofisi ya Elimu Maalum, nambari ya simu 1-888-320-8384.

MICHIGAN Education
UPDATED MAY 2015

Nyenzo hizi zilitengenezwa na ruzuku iliyotolewa na Idara ya Elimu ya Michigan na Idara ya Elimu ya Marekani.

Ninawezaje Kumwandikisha Mtoto Wangu katika Shule ya chekechea?
Mwongozo wa Wazazi # 3

Mtoto ambaye ana umri wa miaka mitano mnamo au kabla ya tarehe 1 Septemba anaweza kuandikishwa kuchukuliwa katika shule ya chekechea*

- Wilaya nyingi za shule za umma huanza kuwachukua watoto wa chekechea mapema katika majira ya kuchipuka kwa majani kwa msimu ufuatao wa kupukutika kwa majani.
- Wasiliana na shule ya eneo lako ili kujua tarehe halisi.
- Ikiwa ungependa kumwandikisha mtoto wako katika wilaya isiyo yako, wasiliana na wilaya hiyo ili kuona kama wanatoa nafasi ya shule za kuwachukua watoto wa chekechea na ikiwa ni hivyo, tarehe ya makataa ya maombi ni lini.
- Kuwa tayari na majina, anwani, na nambari za simu ili kujaza fomu. Pia beba maelezo ya mawasiliano kuhusu daktari wa mtoto wako.
- Wasiliana na shule ya eneo lako kwa maelezo wanayoweza kutaka uyalete.
- Ikiwa huna fomu zote wanazotaka, unapaswa bado kumwandikisha mtoto wako kwa chekechea. Wahudumu wanaweza kukusaidia kupata fomu zozote zinazokosekana.
- Ikiwa unaishi katika makao ya muda au umepoteza makazi yako hivi karibuni, fahamisha shule yako kuhusu suala hilo wakati unamwandikisha mtoto.
- Unapomwandikisha mtoto, fahamisha shule ikiwa mtoto wako anapata huduma nyingine, kama vile matibabu ya kumwezesha kuongea.

Hapa kuna baadhi ya stakabadhi za kawaida zinazohitajika ili kumwandikisha mtoto wako katika shule ya chekechea.

- Thibitisho la umri na utambulisho wa mtoto wako (cheti cha kuzaliwa) kinahitajika. Thibitisho lingine la kuzaliwa linaweza kukubaliwa (pasipoti, rekodi ya hospitali ya kuzaliwa kwa mtoto, rekodi za kuchukuliwa na wazazi walezi au cheti cha ubatizo, n.k.).
- Thibitisho la mahali unapoishi (leseni ya dereva, kadi ya usajili wa mpiga kura, bili ya matumizi, taarifa ya kodi, taarifa ya mlipa kodi, au hati yoyote rasmi inayoonyesha jina na anwani yako).
- Rekodi za chanjo. Unaweza kuwasiliana na shule yako ili kuomba kutopata chanjo hali inayokuruhusu kutopata chanjo kwa sababu za kidini au matibabu.
  Chanjo za sasa zinazohitajika zinaweza kupatikana kwenye Michigan Care Improvement Registry (www.mcir.org).
- Uchunguzi wa kuona na kusikia. Kila mtoto anahitaji kufanyiwa uchunguzi wa kusikia na kuona kabla ya kuanza shule ya chekechea.

Tafadhali angalia Mwongozo wa Wazazi nambari #4 ili upate maelezo kuhusu chaguo la kuandikishwa mapema katika shule ya chekechea.

Nyenzo hizi zilitengenezwa na ruzuku iliyotolewa na Idara ya Elimu ya Michigan na Idara ya Elimu ya Marekani.

Mtoto Wangu Atakuwa Akifanya Nini Katika Shule ya chekechea?
Mwongozo wa Wazazi # 9

Ikiwa mtoto wako ameenda katika shule ya mapema au kituo cha kuwahudumia watoto mchana, shule ya chekechea inaweza kuwa "mabadiliko makubwa."

- Mpango wa chekechea utakuwa rasmi zaidi kuliko shule ya mapema. Shule za siku hizi zina muda zaidi wa masomo ili kutimiza malengo fulani.
- Shule za eneo zinaruhusiwa kuchagua mipango ambayo inatimiza malengo hayo ya masomo. Pia shule huchagua ratiba ya kila siku ya shule ya chekechea.
- Jimbo la Michigan lina malengo ya mafanikio watoto wanapaswa kuwa wamejifunza mwisho wa mwaka wa chekechea.

Uliza mwalimu wa mtoto wako kushiriki ratiba ya kila siku ya chekechea na wewe. Kisha unaweza kuongea na mtoto wako kuhusu sehemu za siku, kama vile:

- Muda wa kushiriki kundi kubwa na ndogo.
- Muda wa watoto kufanya kazi kivyao kwenye miradi au katika "vituo' darasani.
- Muda wa kula vitafunio.
- Chakula cha mchana katika kafeteria.
- Shughuli za utendakazi na utulivu.
- Madarasa ya ziada kama vile mazoezi, muziki, sanaa, maktaba na kompyuta.

Haijalishi ratiba ya chekechea iko aje, jambo muhimu zaidi ni utofauti na aina za nafasi za kusoma.

- Walimu wazuri wanajua kwamba watoto wa chekechea wanahitaji nafasi nyingi za kusoma. Shughuli katika maeneo ya kawaida ya masomo zimejumuishwa pamoja na shughuli za ukuaji wa kihisia na kimwili.
- Kwa kuongea na mwalimu, unaweza kujifunza kuhusu yale mtoto wako wako anayafanya. Hii ni muhimu wakati wa mabadiliko mnapokuwa mkifanya shughuli pamoja ili kumsaidia mtoto wako kuzoea.
- Hii ikifanya kazi, mtoto wako atatazamia kwenda shule kila siku!

Kukua - mabadiliko kutoka kwa miaka ya mapema ya shule. Tofauti ambazo mtoto wako anaweza zipata darasani:

- Muda uliopangwa zaidi na shughuli zinazoongozwa zaidi na mwalimu.
- Miradi zaidi ya kikundi na kutocheza sana kivyake.
- Shughuli zaidi za ndani ya darasa, muda mchache wa kucheza nje.
- Kuandika herufi na nambari zaidi.
- Kanuni zaidi za shule.
- Watoto zaidi darasani.

MICHIGAN Education
UPDATED MAY 2015

Nyenzo hizi zilitengenezwa na ruzuku iliyotolewa na Idara ya Elimu ya Michigan na Idara ya Elimu ya Marekani.

Kwa nini ni Muhimu Kucheza katika Shule ya Chekechea? Mwongozo wa Wazazi # 10

Kuna njia nyingi za kujifunza. Watoto na watu wazima hujifinza vizuri wakati wanahimizwa na wanavutiwa.

Utafiti wa miaka nyingi unaonyesha kwamba kucheza ni zaidi ya burudani na michezo.

Kucheza huongezea kukua vizuri katika maeneo mengi, ikiwa ni pamoja na ukuaji wa:

- **Kiakili:** Kuna uhusiano wa karibu kati ya kucheza na kukua vizuri kiakili. Kucheza huweka msingi wa ufanisi wa baadaye shuleni katika kusoma na kuandika. Hutoa uzoefu ambao huwasaidia watoto kukua.
- **Utangamano:** Kucheza ni muhimu kwa ubunifu. Husaidia pia kukuza ujuzi bunifu wa kutatua matatizo.
- **Kihisia:** Mchezo wa kujiundia vitu ili kujiamini huboresha ujuzi wa kushirikiana na wengine na kuwezeza kuhisi huruma. Michezo huwasaidia pia watoto kujifunza kudhibiti tabia zao.
- **Kimwili:** Ugumu na kung'amua michezo husaidia misuli ya watoto kukua na ubongo kukua.

Kucheza kuna faida nyingine katika kujifunza:

- Watoto wengi wa chekechea hawako tayari kukaa chini na kusikiliza kwa vipindi vya muda mrefu.
- Utafiti unaonyesha kucheza hufanya kazi vizuri wakati mwalimu anatumia uwezo na vivutio vya mtoto. Mwalimu anaweza kutoa nafasi za kusoma kupitia uzoefu.
- Kucheza kwa mtoto mdogo ndio kazi yake. Darasa la chekechea linapaswa kujaa nafasi za kusoma kupitia kucheza.
- Watoto wanapenda shule wakati mwalimu anaunga mkono kusoma kwao ndani na nje ya darasa na wakati wazazi wao wanapendezwa katika siku yao shuleni.

Nyenzo hizi zilitengenezwa na ruzuku iliyotolewa na Idara ya Elimu ya Michigan na Idara ya Elimu ya Marekani.

Ninawezaje Kumsaidia Mtoto Wangu Kutuliza Woga wa Siku za Kwanza?
Mwongozo wa Wazazi # 18

Fikra nzuri husaidia sana.

- Mtoto wako atahisi imani yako katika uwezo wake kufanikiwa.
- Mtoto wako anashawishiwa na mambo unayoyasema na kuyafanya. Pia yeye huona hisia unazoonyesha.
- Ni muhimu kwamba uwe na furaha na umechangamka kuhusu mtoto wako kuanza chekechea. Mtoto wako atafuata uongozi wako.
- Kuna vitabu vingi vizuri vya kusoma pamoja ili kujiandaa kwa siku ya kwanza ya shule.

Kiamsha kinywa ndicho mafuta ya mwili wa mtoto wako.

Njia nzuri ya mtoto wako kuwa na nguvu siku nzima ni kumpa kiamsha kinywa kizuri. Chakula hiki ni muhimu kwa sababu mwili wa mtoto wako unahitaji "mafuta" ili kufanya kazi asubuhi. Tafiti nyingi zimeonyesha kwamba watoto wanaokula kiamshakinywa kila asubuhi wana rekodi nzuri shuleni na fikra nzuri. Nguvu inayotokana na kula kiamsha kinywa kizuri pia husaidia na kukuza kumbukumbu ya mtoto.

Maamuzi humwezesha mtoto wako.

Mruhusu mtoto kufanya maamuzi kuhusu mavazi ya shule, chakula na vifaa vya shule. Hii inaweza kumsaidia kuhisi mjasiri zaidi na mwenye usukani. Pia hii huongezea ujuzi wake wa uhuru.

Mnaweza kuepuka saa za asubuhi zenye shughuli nyingi.

- Kuamka ukiwa na muda wa kutosha wa kujiandaa kwenda shule hufanya nyumba yako kuwa tulivu zaidi. Hii husaidia mtoto wako kuhisi ametulia zaidi.
- Kupanga nguo na vifaa usiku hufanya kazi vizuri kwa familia nyingi.

Kusema kwaheri ni vyema kuliko "kupotea."

- Kumwacha mtoto wako siku hiyo ya kwanza huenda ikawa vigumu. Tafiti zimeonyesha kwamba kwaheri ya upendo na thabiti ndio njia nzuri ya kwenda.
- Mtulize na umjulishe kuhusu wakati mwingine atakapokuona. Usimfanye mtoto wako ahisi vibaya wakati anaekasirika kukuona ukienda.
- Mwalimu anaweza kusaidia na maelezo mazuri kabla ya siku ya kwanza ya shule.

Nyenzo hizi zilitengenezwa na ruzuku iliyotolewa na Idara ya Elimu ya Michigan na Idara ya Elimu ya Marekani.

Ninawezaje Kuhusika na Elimu ya Mtoto Wangu? Mwongozo wa Wazazi # 20

Kuhusika katika elimu ya mtoto wako.

Kuhusika kwa mzazi humsaidia mtoto wako kufanikiwa shuleni. Husababisha mtoto wako kutokosa shule sana na kuwa na tabia nzuri. Nyumba ambayo inaunga mkono kusoma ni muhimu. Hii huathiri ufanisi wa shule wa mtoto wako. Ni muhimu zaidi ya kipato chako, kiwango cha elimu au utamaduni wako na inafurahisha.

Mambo matatu ambayo humsaidia mtoto wako kufanikiwa shuleni.

1. Saidia kupanga muda wa mtoto wako.
2. Saidia na kazi ya nyumbani.
3. Ongea kuhusu shule.

Vidokezo vifuatavyo vinaweza kumsaidia mtoto wako kufanya vyema:

- Anza ratiba ya kila siku ya familia. Toa muda na mahali patulivu pa kusoma. Kuwa imara kuhusu wakati wa kulala. Kuleni chakula cha jioni pamoja
- Weka vikwazo vya kutazama TV. Weka shughuli za baada ya shule na ufuatilie.
- Onyesha thamani ya nidhamu na kufanya kazi kwa bidii.
- Gundua na uunge mkono talanta maalum.
- Shiriki ufanisi na familia na marafiki.
- Ongea mambo mazuri kuhusu uzoefu wa shule.

Njia tofati za kuhusika:

MAWASILIANO: Soma na ujibu ilani na barua zote. Hudhuria makongamano ya wazazi na walimu. Watafsiri wanaweza kupatikana wakihitajika.

KUJITOLEA: Unga mkono darasa la mtoto wako kwa kumsaidia mwalimu wao. Nenda kwenye safari ya nje. Shiriki utamaduni wa familia yako na watoto wengine.

UONGOZI WA WAZAZI: Jiunge na PTA/PTO au makundi mengine ya wazazi. Makundi haya hutoa nafasi nyingi za kusaidia shuleni. Hukupa pia nafasi ya kuungana na wazazi na wahudumu wengine.

KUTOA MAAMUZI: Mruhusu mwalimu mkuu kujua kama unataka kuhudumu katika baraza au kamati za ushauri.
Hudhuria mikutano ya bodi ya shule au vikao vya kazi.

Ikiwa wewe ni mzazi wa mtoto mwenye ulemavu, hakikisha umejumuishwa katika ukuzaji wa Mpango Uliobinafsishwa wa Elimu (IEP). Kuhusika kwako ni muhimu kwa mchakato wa IEP.

MICHIGAN Education
UPDATED MAY 2015

Nyenzo hizi zilitengenezwa na ruzuku iliyotolewa na Idara ya Elimu ya Michigan na Idara ya Elimu ya Marekani.

Je, kuna vitabu vya kusoma vya kumsadia mtoto wangu kujiandaa kwa shule ya chekechea?

Ndiyo! Hapa kuna baadhi ya vitabu vya kufurahisha ambavyo vinaweza kumsaidia mtoto wako kufahamu ratiba ya chekechelea.

Monkey: Not ready for kindergarten **by Marc Brown** ISBN: 9780553496581
Familia ya tumbili huonyesha njia nzuri ya kijamii ya kujiandaa kwa shule ya chekechea.

Kindergarten rocks **by Katie Davis** ISBN: 9780152064686
Dexter hana wasiwasi kuhusu kuanza shule ya chekechea, lakini mbwa wake wa kuchezea, Rufus, ana wasiwasi sana.

Kindergarten diary **by Antoinette Portis** ISBN: 9780061456916
Annalina anaelezea mpito wake hadi shule ya chekechekea kwa kuweka rekodi ya mwezi wake wa wanza shuleni.

Welcome to kindergarten **by Anne Rockwell** ISBN: 9780802776648
Mtazamo rahisi, wa kusaidia wa taratibu za shule ya chekechea.

Planet kindergarten **by Sue Ganz-Schmitt** ISBN: 9781452118932
Mtoto anafikiria akienda shule ya chekechea kuwa ni safari ya kwenda sayari nyingine

Miss Bindergarten gets ready for kindergarten **by Joseph Slate** ISBN: 9781442053038
Kitabu hiki maarufu cha alfabeti ya wanyama huonyeshwa kwa werevu jinsi walimu wanavyowandaa wanafunzi wakati wanafunzi wanajiandaa kwenda shuleni.

Is your buffalo ready for kindergarten? **by Audrey Vernick** ISBN: 9780062067197
Mtazamo wa kufana na wa kusaidia wa wasiwasi wa siku ya kwanza, hadithi hii inafuatilia nyati katuni anayejifunza kwamba kuna nafasi ya kila mtu katika shule ya chekechea.

Timothy goes to school **by Rosemary Wells** ISBN: 9780140567427
Katika hadithi hii maarufu ya kuanza shule Timothy anajigunza kuhusu kukubaliwa na kupata marafiki wapya.

How do dinosaurs go to school? **by Jane Yolen** ISBN: 9780439020817
Huelezea jinsi dinosari ndogo zinapaswa kufanya wakati wa siku ya kawaida ya shule.

Mom, it's my first day of kindergarten! **by Hyewon Yum** ISBN: 9780374350048
Katika mtazamo wa kupendeza mama ana wasiwasi zaidi kuhusu shule kuanza zaidi ya mtoto wake. Kitabu kizuri cha kuanzisha mazungumzo kuhusu hisia za wazazi na watoto kuhusu shule ya chekechea.

Capital Area District LIBRARIES

Pata vitabu hivi na vingine ving katika tawi lako la CADL au kwenye tovuti yetu: cadl.org.

Je, huna kadi ya maktaba? Tembelea tawi lolote la CADL au cadl.org ili kujua jinsi ya kupata moja.

***Maktaba ya Umma ya East Lansing inawahudumia wakazi wa East Lansing: elpl.org.**